

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

SHULE YA SECONDARI MANDAKA

S.L.P 301,

MWANGA.

Kumb Na MSS/JI/KI/2020

JINA LA MWANAFUNZI

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI
MANDAKA, WILAYANI MWANGA, MKOANI
KILIMANJARO KWA MWAKA WA MASOMO 2021**

1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha kwanza. Mhula wa masomo utanza tarehe 11/01/2021. Tafadhali hakikisha unaripoti siku hiyo. Endapo hutaripoti hadi ifikapo tarehe 22/01/2021 nafasi yako itachukuliwa na nwanafunzi mwingine mwenye uhitaji.

2. MAMBO MUHIMU

2.1 Sare za Shule

2.1.1 Wavulana

- Suruali mbili za damu ya mzee zisizo bana na lazima ivaliwe na mkanda mweusi usio na bakoli kubwa.
- Mashati mawili meupe mapya yenye mikono mifupi yasio bana.
- Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili, visiwe vimechongoka, buti wala raba na viwe vya kubrashi.
- Soksi nyeusi ndefu pea mbili.
- Tai mbili ndefu za kufunga, damu mzee (kitambaa esterm).
- Sweta damu ya mzee, ifanane na sare ya suruali.

2.1.2 Wasichana

- Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee, rinda box yenye mapindo mawili pembeni, mbele na nyuma, iwe ndefu lakini isiyoburuza chini.
 - Mashati mapya meupe mawili, tetron mikono mifupi na yasio bana.
 - Tai ndefu rangi ya damu ya mzee ifanane na sketi.
 - Viatu vyeusi vya kamba pea mbili, visiwe na kisigino kirefu. Simpo, raba, na buti haviruhusiwi.
 - Soksi nyeupe ndefu zinazo fika magotini (stocking).
 - Sweta damu ya mzee
- NB Sare za michezo kwa wote ni tshirt rangi damu ya mzee na raba rangi yeyote..

Kumbuka. Nguo/sare zitakazo shonwa vibaya au kutofautiana rangi hazitoruhusiwa.

2.2 Vifaa Vingine

- Daftari kubwa 10.
- Kalamu blue au nyeusi.
- Mathematical set yenye vifaa vyote (compas).
- Dictionary (English to English).
- Daftari ndogo zisizopungua 10 kwa ajili ya mazoezi.
- Graph paper moja (pad moja)

2.3 Vifaa vya Usafi na Mazingira

2.3.1 Wasichana

- Ndoo kubwa moja mpya yenye mfuniko.
- Ufagio wa ukindu mmoja.
- Ufagio mrefu wa chelewa.

2.3.2 Wavulana

- Ndoo kubwa moja mpya yenye mfuniko
- Ufagiommoja wa ukindu.
- Hard broom moja na soft broom moja.

NB Mpatie mwanao mkoba mzuri (begi) kwa ajili ya na kubebea na kutunzia madaftari, kijiko pamoja na sahani. Tafadhali jukumu la kumwandikisha mwanafunzi shuleni ni la mzazi. Hivyo mzazi mlete mwanao na kuhakikisha anaandikishwa kiusahihi. Mwanafunzi asiyekuja na mzazi/mlezi hatopokelewa.

3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za elimu, nyaraka na miongozo yote na utekelezaji wake chini ya ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

- a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila kazi ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kikamilifu kafanya maandalia ya masomo (preparation).
- d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za uma.
- j) Kutopiga kelele darasani.
- k) Hauruhusiwi kufuga nywele, ndevu, kunyoa vibaya, kuwa na kucha ndefu, kupaka rangi wala kusuka nywele.
- l) Hauruhusiwi kuongea lugha nyingine zaidi ya kiingereza wakati wote uwapo shuleni.
- m) Unapaswa kuvaa sare ya shule kikamilifu (Hauruhusiwi kutochomekea shati wala kuvaa mlegezo).
- n) Hauruhusiwi kuwa na simu, redio, au line ya simu shuleni.

- o) Huruhusiwi kuja na chakula shule. Kila mwanafunzi atakula chakula cha mchana shuleni kulingana na makubaliano ya wazazi.
- p) Huruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali.

3.1 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa Shule au Kusimamishwa Shule

- a) Wizi wa aina yoyote
 - b) Uasherati na ushoga.
 - c) Ubakaji.
 - d) Ulevi, sigara na utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
 - e) Kupigana au kupiga na matumizi ya lugha za matusi shuleni.
 - f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
 - g) Kudharau Bendera ya Taifa /wimbo wa Taifa.
 - h) Kuwa mjamzito/kumpa mimba mwanafunzi.
 - i) Kuoau au kuolewa.
 - j) Kutoa mimba.
 - k) Utoro.
 - l) Kuhamasisha au kushiriki katika migomo.
 - m) Kugoma au kuto waheshimu walimu na watumishi wengine.
- Nakutakia maandalizi mema.**

KARIBU SANA MANDAKA SEKONDARI

.....

MKUU WA SHULE

FOMU YA MAKUBALIANO

Mimi(Jina la mwanafunzi)

Kidato

Nakiri kwamba, nimesoma kwa kina sheria na taratibu za kujiunga na shule hii na kuzielewa. Nakubali kuzitekeleza kwa wakati wote nikiwa mwanafunzi na kuzilinda. Natambua kuwa hizi ndizo zitakuwa mwongozo wangu wa kunifanya niishi shuleni kwa amani na kuwa na mafanikio katika masomo yangu. Nina tambua kuwa kuvunja sheria ni kukiuka taratibu za shule na nitakuwa tayari kupokea adhabu inayostahili.

.....

Sahihi ya mwanafunzi.

Mimi(Jina la mzazi/mlezi) wa

..... kidato.....

Ninakubaliana na sheri na taratibu za shule, na ninahidi nitakuwa mstari wa mbele kushirikiana na waalimu/walezi ili kuhakikisha mwanangu anazifuata sheria za shule. Nina ahidi kumpatia mahitaji yote likiwemo hitaji muhimu la chakula cha mchana ili kulinda afya, nidhamu na taaluma ya shule.

.....

Sahihi ya mzazi/mlezi

.....

Tarehe

